

Vipindi vya Kusikiliza vya Familia

# Ruzuku ya Maendeleo ya watoto ambao hawajafika umri wa kuanza shule

## Humanitarian Assistance with Kindness & Interculturalism Msaada wa kibinadamu wenye kuzingatia utu na ujamaa

Mwezi Januari, 2020, kipindi cha usikilizaji kilichowahusisha wazazi na walezi kiliandaliwa katika kituo cha Msaada wa kibinadamu (Humanitarian Assistance with Kindness & Interculturalism—HAKI) katika Ziwa Oswego, Oregon. Kipindi hiki cha kusikiliza kilikuwa ni sehemu ya mfululizo wa vipindi vya usikilizaji vya familia vilivyofadhiliwa na Ruzuku ya Maendeleo ya Utotoni kama sehemu ya tathmini ya mahitaji ya elimu ya utotoni. Kipindi cha kusikiliza kilibuniwa, kupangwa na kuandaliwa na HAKI pamoja na wawezeshaji wa Kitamaduni wa AB kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Jimbo la Portland na OSLC Developments, Inc. Madhumuni ya vipindi vya usikilizaji lilikuwa kujumuisha mitazamo ya familia za wahamiaji na wakimbizi wa Kiafrika, kuelewa mahitaji yao ya elimu ya awali na uzoefu wao, na hatimaye kuhabarisha mpango wa maendeleo wa elimu ya utotoni ya jimbo. Kipindi hiki cha usikilizaji kilifanywa kwa lugha ya Kiswahili kikiwahusisha wazazi na walezi 13—kina mama 10 wa watoto wadogo, kina baba wawili, na bibi mmoja. Isitoshe, baadhi ya wazazi walioshiriki pia walikuwa na uzoefu katika suala zima la elimu ya utotoni kama mwalimu, mgeni wa kuzuru nyumbani, au mwalimu wa mzazi.

### Kwa sasa ni nani anayewaangalia watoto wako wa umri wa miaka kati ya 0-5 na ni shughuli gani wanazofanya?

Kupata usaidizi kutoka kwa wazazi wao na/au wanafamilia wengine ilikuwa ni jambo la kawaida kwa wazazi hawa wote. Wazazi watano walikuwa na watoto wadogo katika daraja la awali au mwanzo wa daraja la awali, na wawili kati ya wazazi hao walikuwa na mwalimu au mgeni anayezuru nyumbani anayezungumza Kiswahili na anayetoka katika jamii yao. Walipoulizwa aina ya shughuli ambazo watu hawa huwapa watoto wao wadogo, wazazi waliongelea mamba mbalimbali ikijumuisha muda wa kuangalia runinga, michezo ya kuigiza, wakati wa kutoka nje, wakati wa kula, kulala, kufanya sanaa na ufundi, kusoma, kuweka ratiba, kujenga stadi za kihisia na kimahusiano, kuhesabu, kujifunza rangi, maumbo, herufi na kujumuika na marafiki.

> “Mlezi huyu huzungumza Kisomali na Kiswahili; yeye huwaongelesha watoto wadogo Kiswahili. Yeye husimulia hadithi kuhusu Afrika kwa Kiswahili.”

Walipoulizwa mambo wanayofanya watoa huduma ili kusherehekea au kufanya mila, tamaduni, na lugha ya watoto wao, wazazi walisema kuwa wao, wanafamilia au wanajamii huwaongelesha watoto wao Kisomali au Kiswahili, na huwasimulia hadithi na kuwaimbia nyimbo watotot kwa lugha ya Kiswahili ili wasipoteze lugha yao ya nyumbani. Wao hufanya mila za Kiislamu kama vile kuwaosha watoto baada ya kufika nyumbani wakitoka shuleni, kusoma Korani, na kuwafundisha watoto kusali.

## Manufaa ya Mipango ya Elimu ya Utotoni

Wazazi walio na watoto walio katika Daraja la Awali au Mwanzo wa Daraja la Awali walizungumza kuhusu faida kwa familia zao, ikijumuisha kushuhudia watoto wao wakitumia maneno kuelezea hisia na kupewa rufaa ya mtaalamu wa usemi. Mzazi mmoja alisema kuwa mtoto wake ambaye alikuwa katika mipango yote miwili alionekana kupata maarifa zaidi kuliko mtoto wake ambaye alihudhuria mpango wa Daraja la Awali pekee. Mzazi mwingine alizungumza kuhusu thamani ya kuwa na mtaalam anayetembelea kaya.

"Watu wengi hujisikia kutokuwa huru au hutatizika kuwakaribisha wageni nyumbani. Wao hutusaidia na masuala ya kukawia mapema ambayo mtaalam anayetembelea kaya/ nyumbani anaweza kutoa rufaa kwa mtaalam. [Watembeleaji waNyumbani] husaidia shughuli na [sisi] tulipata huduma bora. Awamu zote za ukuaji kuhusu uwezo wa kusikia, kuzungumza, hisia na mahusiano, utambuzi, kimwili. Kama nikizungumza na mtoto wangu mdogo, awali sikuzungumza na mtoto wangu, sasa ninazungumza naye, na hata kama hana maneno, anaiga."

Mzazi mmoja, ambaye pia ni mtoa huduma elimu ya utotoni, alieleza kuwa katika jamii yake, wazazi wengi hufikiria kuwa watoto wadogo hawajifunzi chochote wanapokwenda shule ya utotoni kwa sababu ya msisitizo wa michezo kwenye shule hizi. Hata hivyo, alitaja manufaa ya michezo na hatua nyinginezo za kujifunza zinazofanywa katika shule za awali.

"Kunaweza kuwa na vifaa vingi vya kuchezea katika darasa la shule ya awalilakini muhimu zaidi wanachojifunza ni stadi za kihisia...Lakini pia tunawafundisha kuhesabu, kutambua rangi, maumbo, herufi, tunawaandalia kwa ajili ya ya chekechea. Mazungumzo sambamba, kukutana na na marafiki; amini usiamini, wanajifunza mambo mengi sana. Tunatumia vifaa vya kutazama, hisia; tunawapa maneno ambayo bado hawawezi kuchakata."

## Ni usaidizi gani wa elimu ya utotoni ambayo ungependa kumpa mtoto wako ili kumwandaa kwa ajili ya chekechea?

Wazazi wengi walisema kwamba wangependa pawe na darasa lenye misingi ya kitamaduni au mpango wa elimu ya utotoni katika jamii yao, na walitaja kutokuwepo kwa nafasi za watoto kuhusiana, kama vile wakati wa kusimulia hadithi, ambapo utamaduni, lugha, na maadili yao yataeleweka, kuzingatiwa na kutekelezwa. Wazazi kadhaa walipendekeza kuwa HAKI ingetoa aina hii ya usaidizi. Mzazi mmoja alizungumzia umuhimu wa mipango ya lugha mbili ili watoto waweze kujenga ujuzi wa kubadilisha matumizi ya lugha moja hadi nyingine. Mzazi mwingine alisema kwamba angependa kuona uelewa zaidi na marekebisho ya maudhui yanayofundishwa katika elimu ya utotoni kulingana na dini yake kwani wakati mwingine shule hufundisha watoto mambo ambayo huenda kinyume na dini yao. Wazazi wote walisema kwamba wangependa mtaalam anayezuru nyumbani au mtoa huduma anayezungumza lugha yao na anayefahamu utamaduni wao, na anayefanya kazi huku akielewa kwa nini familia zinaweza kusita kushiriki katika usaidizi wa elimu ya utotoni inayotawaliwa na wazungu. Wazazi wachache walitaja kwamba kukosa kuwaamini watoa huduma na waalimu wa nje ya jamii yao kulikuwa kizuizi cha ushiriki katika fursa za elimu ya utotoni.

"Wazazi wengi huogopa kukiwa na mtaalam anayezuru nyumbani Mmarekani. Hii ni kwa sababu wanahofia kuwa watawasiliana na DHS. Watu wengi hawataki hivyo, na hivyo hupoteza nafasi nyingi. Ni vigumu kumwamini mtu wa nje ya jamii yako kuja nyumbani kwako au kumwalika nyumbani mwako. Familia au watoto wote wanaweza kuchukuliwa. Hata kama mtoto akianguka au kuumia, wataalam hawa wanaweza kuwalaumu wazazi. Uaminifu ni suala kubwa. Jamii hii ina EHS lakini hawashiriki kwa sababu hawawaamini watu wa kutoka nje ya jamii yao."

Kwa wazazi ambao walitaka kupokea usaidizi wa nje ya nyumbani kwao, kulikuwa na mapendekezo mbalimbali, ingawa tarehe na saa ambazo walihitaji zaidi zilijumuisha siku za mwisho wa wiki na alasiri baada ya saa saba mchana, kwa kuwa wazazi wengi hufanya kazi zamu ya adhuhuri na usiku. Wazazi watatu walisema kuwa usaidizi wa elimu ya utotoni ungefanyika siku mbili kwa wiki, mzazi mwingine akasema mara moja kwa wiki au mara mbili kwa mwezi kwa watoto wa umri wa miaka 3-5. Mzazi mwingine alisema madarasa ya asubuhi yanafaidazaidi kwani watatarajiwa kuanza ratiba ya asubuhi wakati wakiingia shule ya chekechea. Mzazi mmoja alisema "Tunapenda watoto wetu wasalie nyumbani kwa kuwa hatuwaamini wahusika. Tungependa tu wanafamilia wawalee watoto wetu wadogo."

## Ni Usaidizi Gani wa Malezi Ambao ni Muhimu Zaidi?

Wazazi walikuwa na maoni mengi kuhusu usaidizi ambao ungewafaa. Wazazi walisema kwamba mara nyingi wanahisi kutengwa na wangejisikia huru zaidi kujifunza wakiwa katika mazingira yanayozingatia tamaduni na rika lao.

"It is like day and night. That's why they're always having problems with their teachers. The teacher is expecting them to act differently." In families' countries of origin, children are expected and taught to respect their teachers differently. Children are taught to respect teachers just as much as they are taught to respect their parents."

Isitoshe, kuwa na mtu wa jamii yao anayeweza kuwafundisha wazazi kuhusu awamu mbalimbali za ukuaji, kuwawekea ratiba watoto wadogo, na shughuli tofauti wanazoweza kufanya na watoto wao. Wazazi pia walizungumza kuhusu faida za kuwa na mwalimu au mkufunzi wa wazazi anayezuru jamii yao na kuzungumza na wazazi kuhusu jinsi wanavyoweza kuwandaa watoto wahudhurie shule, matarajio kwa watoto na kwa wazazi, na jinsi ya kuwasiliana na walimu.

"Kama mzazi, ikiwa hujaelimika huwezi kuyatambuamambo hayo madogo muhimu. Sharti upate elimu na utambue kuwa unajifunza katika umri huo mdogo na hili ndilo jambo linalowaathiri kama watu wazima. Mambo madogo unavyofanya nyumbani, shughuli ndogo zinawatambua na kuwaunganisha. Anajifunza kitu au ukuaji wake sasa ni tofauti sana namiezi mitatu baadaye."

## Tofauti kati ya Utamaduni wa Nyumbani na Utamaduni wa Shuleni

Wazazi walisema wazi kuwa watoto wao wamelelewa katika tamaduni na mila tofauti nyumbani kwao kando na utamaduni wa uzungu shuleni mwao. Wazazi walieleza kuhusu changamoto zao na za watoto wao wanapokabiliana na tofauti hizi za kitamaduni. Mzazi mmoja alisema, "Tofauti hizi ni kama usiku na mchana. Ndiyo sababu daima huwa na shida na walimu wao. Mwalimu anawatarajia wawe na tabia tofauti." Katika nchi za asili za familia, watoto wanatarajiwa na hufundishwa kuwaheshimu walimu wao kwa njia tofauti. Watoto hufundishwa kuheshimu walimu sawasawa na walivyofundishwa kuwaheshimu wazazi wao.

"...watoto huwaogopa walimu wakiwa nyumbani. Walimu hapa hawana nidhamu sawa. Hapa wazazi wanawajibika kwa nidhamu hiyo."

"Shuleni [mtoto] anaweza kumwambia mwalimu, Siko tayari, ninahitaji mahali patulivu kwa sababu siko tayari kukusikiliza. Katika utamaduni wetu,nyumbani kwetu, watoto sharti wawasikilize watu wakubwa."



### Haja ya Kuwafundisha Walimu Kuhusu Utofauti

Familia zilipendekeza suluhisho moja linalowezekana, ambalo linaweza kusaidia walimu kuelewa tofauti kati ya tofauti za kitamaduni za wanafunzi nyumbani na shuleni ni kuwafundisha walimu kuhusu utofauti hizo. Walimu wanawatarajia watoto kutoka jamii hii kuwa na tabia tofauti na wanazotarajiwa kuwa nazo nyumbani.

"Nadhani tunapaswa kuwaelimisha walimu kuhusu utamaduni wetu...Wanapaswa kupewa na siku ya mapumziko kwa ajili ya kupewa mafundisho kuhusu tamaduni mbalimbali; tamaduni za Kiswahili, Kisomali na Kiafrika kwa jumla. Tunachofanya nyumbani na tunachofanya shuleni, na walimu wanapaswa kuja na ikiwa wana maswali yoyote wanapaswa kufundishwa kuwapigia wazazi simu kwanza kabla ya kupigia DHS."

"Tamaduni yetu ina ukali fulani, kwa hivyo inabidi tuwaelewe watoto wetu kwa sababu walimu hutumia maneno fulani wakiongea. Kama wazazi tunahitaji [kuelewa] kuwa pia tunaweza kuzungumza kwa sababu utamaduni wetu haufundishi kuwa...Kwa hivyo jifunze jinsi ya kuzungumza nao na kuwasikiza na kuwapa nidhamu. Unaweza kufanya hivyo kwa kutumia tu maneno yako...Kwa hivyo tunahitaji kuwaelimisha wazazi wetu ili tuweze kuwa pamoja na walimu na kuhakikisha kuwa tunaafikiana nao."

Wazazi wachache walikuwa na hofu ambayo wazazi katika jamii hii huwa nayo, kuwa walimu watawasiliana na DHS, kwa sababu ya matukio ya awali yanayoonyesha kutokuelewana kwa kitamaduni. Mzazi mmoja alisema kuwa shuleni watoto hufundishwa kwamba ikiwa wanadhulumiwa, wanapaswa kupiga simu namba 911 au kuwasiliana na walimu wao.

Watoto…"wanasema, 'Ukiniambia hivyo, mwalimu alinishauri nipige simu namba 911 kukushtaki.' Kwa hivyo kwetu, tunapozungumza na watoto wetu, wakati mwingine inabidi tuseme 'Basi, wacha!' Kwahiyo tukisema hivyo wanachukulia kama dhuluma na kusema, tutapiga simu kwa 911." Suala hili huchanganya zaidi kwa sababu wazazi huogopa kwamba walimu watachukua maelezo haya, wapige simu kwa DHS, na familia itaingia mashakani katika mfumo wa masuala ya watoto. Wazazi walisema kuwa walimu wanapaswa kuwasiliana na familia kuhusu hoja yao kabla ya kuwasiliana na DHS.

## Matukio ya Ubaguzi na Dhana Potovu kutoka kwa Walimu na Shule

Familia hizi zilishirikisha mifano mingi kuhusu matukio ya ubaguzi. Mzazi mmoja alisema "Hii ndiyo changamoto kubwa zaidi, ubaguzi. Ubaguzi huanza katika miaka ya kwanza ya utotoni na unaweza kuendelea baadaye maishani." Wazazi wameshuhudia walimu wakiwatendea watoto wao tofauti kielimu ikilinganishwa na watoto wengine darasani; watoto wameshuhudia kuna viongozi wa shule wanaowaambia watoto mambo mabaya; na wazazi wamebaguliwa wazi na wazazi wengine kwa msingi wa rangi yao.

"Mwalimu mmoja mkuu, yaani hata sio mwalimu, ambaye alimwita mtoto wangu ni mjinga. 'Wewe ni Mwafrika, nyie Waafrika ni wajinga.' Nilishangaa na kuuliza, Alikwambia hivyo yaani alimaanisha? Nilikwenda kwa mwalimu huyu mkuu na kuongea naye akasema 'Ah, sikumaanisha hivyo.' Hapana, haijailishi ulichomaanisha, ulimwambia mwanafunzi kitu na anahisi 'Mwalimu mkuu alisema hivyo.' Hili sio jambo zuri hata! Hupaswi kusema hivyo, hasa ukiwa mwalimu mkuu, kwa sababu wanaamini kuwa unajua zaidi ya walimu wa kawaida. Sikuamini. Sikupenda. Mtoto wangu ambaye alikuwa na umri wa miaka minne hivi, nilimtoa shuleni."

"Kwahiyo hii ndiyo changamoto kubwa zaidi kwa wazazi, yaani ubaguzi unaofanywa na walimu, na wazazi. Nakumbuka siku moja nilikuwa nikipakua chakula cha mchana ambapo palikuwa na watoto kumi mezani. Wazazi fulani waliingia na kusimama karibu na mtoto fulani aliyeketi hapo na kuuliza 'Mtoto huyu anatoka Somalia, yeyena mama na baba yake?' Nikasema ndiyo. 'Basi alipata vipi nywele hizi?' Nikashangaa sana! Kwanza kabisa, kuna Wasomali wengi wenye nywele za aina nyingi."

Mtoto mmoja alipokea viatu kutoka kwa Mwalimu Mkuu wa daraja la awali. Mzazi alifikiri kwamba mwalimu huyo alichukulia kuwa mzazi na mtoto wake ni maskini na hawana vitu hivyo. Jambo hili, pamoja na kwamba Mwalimu Mkuu huyu alifanya hivi bila kuwasiliana na mzazi kwanza lilikuwa changamoto kama tulivyosikia kutoka kwa wazazi wengi—walimu hawafanyi juhudi kuzifahamu familia, au hawafanyi juhudi za kuboresha mawasiliano baina ya wazazi na walimu.

"Ukosefu wa heshima hiyo ya uhusiano wa mzazi na mwalimu hivi kwamba aseme 'Naomba kumpa mtoto wako viatu hivi' Na kunipa fursa ya kusema, Hapana, huwezi kumpa viatu hivyo, au Sivitaki. Unaelewa inachomaanisha? Kudhani kuwa anavihitaji kwa sababu yeye ni Mwafrika au yupo katika mpango wa Head Start ni kukisia mambo yasiyo sahihi."

## Mawasiliano Duni Baina ya Walimu na Wazazi Yanaathiri Familia

Wazazi wengi walishirikisha mifano ya ukosefu mkubwa wa mawasiliano yanayowahusu walimu Wazungu wa watoto wao, na walibainisha kuwa mara nyingi hawapati kiasi sawa cha maelezo kama wazazi wengine wanavyopata (wasio wa Kiafrika). Wazazi wawili walikumbwa na hali ambapo watoto wao walijeruhiwa na walihisi kuwa mwalimu hakuchukua hatua mwafaka au inayotosha.

"Nilimpeleka [mtoto wangu] hospitalini ambapo madaktari waliniarifu kuwa amevunjika. Nilidhani hakumwambia mtu yeyote kwa sababu sikupigiwa simu, sikutumiwa barua pepe; sikupokea chochote. Aliniambia, "Ndiyo, nilimwambia mwalimu kwamba mkono wangu ulikuwa unauma, lakini aliniambia niende niketi kwenye dawati langu."…Kilichonifanya nikasirike na kughadhabika zaidi ni kwamba mtoto wangu ana rafiki wanaokwenda shule moja…ambao ni Wazungu. Nilizungumza naye [mama yake] kuhusu suala hili. Aliniambia, 'Yeye [mwalimu] hunitumia barua pepe kila wakati msichana wangu anapopatwa na tatizo.'…Ndipo nilifahamu dhahiri kuwa palikuwa na ubaguzi."

Mzazi mwingine aligundua kuwa mwalimu wa Head Start alikuwa akitegemea zaidi mawasiliano ya maandishi kuwasiliana na wazazi, ingawa wazazi wengi wa darasa hili hawakuweza kusoma Kiingereza. Hata hivyo, kwa sababu ya mila na matarajio ya kitamaduni ya familia nchini Marekani, wazazi ambao ni wahamiaji na wakimbizi huenda wasilalamike kuhusu suala hilo papo hapo kwa wafanyikazi katika mashirika au taasisi zinazotawaliwa na wazungu, haswa ikiwa hawajajaribu kujenga uhusiano na familia na kuelewa mitazamo yao.

"Nilikuwa msaidizi tu, wazazi wengi wanaotoka katika mila yetu hawapendi kulalamika sana. Tuna uvumilivu sana. tunastahimili mambo mengi. Mara nyingi sisi huzungumza mambo yakiharibika kabisa. Sisi tunaona mambo mengi sana lakini tunabaki kimya tu. hilo ndilo nilililoligundua."

Mzazi mmoja alielezea shida inayosababishwa na walimu wenye mtazamo duni kuhusu familia: "Walimu hushinda na watoto wetu zaidi ya sisi, lakini bado walimu wanajaribu kuwalaumu wazazi, badala ya wazazi kuwalaumu walimu...Lakini bado tunataka kufanya kazi pamoja na walimu, kwa hivyo tunatarajia walimu washirikiane na sisi kuwajumuisha watoto. Kwahiyo kuna ubaguzi unaofanyika katika shule zetu, na ukishughulikiwa kutoka juu mambao yatabadilika."

## Wazazi Wanataka Walimu Zaidi Wanaoelewa na Kuakisia Jamii Yao

Kando na elimu na mafunzo zaidi ya mwalimu/watoa mafunzo na elimu ambayo huwezesha uelewa maalum kuhusu tamaduni mbalimbali, njia nyingine za kutatua mzozo huu zinahitajika, kama vile kuwa na watoa huduma wanaofahamu tamaduni za wanao wahudumia. Mzazi mmoja ana mtoto mmoja anayefunzwa na mwalimu kutoka jamii yao, na mtoto mwingine mkubwa anayefunzwa na mwalimu mzungu Mmarekani, na mzazi huyu alibaini tofauti kubwa kati ya watoto hawa:

"Wakati huu, [mtoto wangu mdogo zaidi] anafunzwa na mtu wa jamii yetu. Akifanya makosa, mwalimu huyo atakuja kunitaarifu. Hawezi kukosa nidhamu shuleni kwa sababu anajua kuwa nitaambiwa na mwisho wa siku nitamuuliza. Atamjali kwa sababu anamfahamu binafsi...Hatasema mtoto wako ni mbaya, atauliza, tunaweza kufanya nini ili kushirikiana kutatua hali hii...Tutashirikiana, tunaelewa wapi tunakotoka...mwalimu na mzazi wanaweza kuwasiliana kwa njia gani, kushirikiana ili kuwasaidia watoto wetu? Hawafai kuwalaumu...lakini [mtoto wangu mkubwa zaidi] anapokosea, ninapokea barua pepe mbaya ikisema mtoto wako alifanya hivi na vile. Hatajitolea na kusema, Nitazungumza nawe kwa sababu hili halifai."

Matarajio ni wanafunzi watoto watakuwa na walimu wengi zaidi wanaoendana na jamii yao, tamaduni na lugha—hata hivyo, kuna changamoto. "Ikiwa kuna shule katika jamii yetu, basi tunahitaji kuwa na walimu wetu. Ninaelewa kuwa kuna suala kuhusu malipo na ndio maana wanaendakutafuta kazi nyinginezo ambazo ni bora."

## Maangazio Muhimu

- Wazazi wangependa kuona vikundi vya kuwasaidia wazazi, elimu ya wazazi, fursa za mahusiano ya watoto, na huduma za kutembelewa nyumbani ambazo hutolewa na mashirika ya jamii na watu kutoka jamii yao, na wenye ufahamu wa tamaduni na lugha yao.
- Watoto wakifunzwa na mwalimu wa jamii yao hupata mazingira saidizi zaidi, na mawasiliano bora ya wazazi na walimu. Hata hivyo, malipo ya walimu yanahitaji kuboreshwa ili kuwavutia watu kutoka katika jamii yao wajiunge na taaluma ya ualimu.
- Suala la ubaguzi unaofanywa shuleni na walimu linapaswa kutatuliwa kutoka ngazi za juu.
- Walimu na wafanyakazi wa shule wanahitaji kufunzwa tamaduni za watoto wakiwa darasani. Walimu wanahitaji mafunzo ya kina yakukabiliana na ubaguzi wa rangi, hasa kuhusu kuelewa na kuwasiliana na wazaziwa asili tofauti nao.
- Kuimarisha mawasiliano na uhusiano na wazazi, ambao unazingatia tamaduni na hujenga kuaminiana ni jambo la msingi katika kuwashirikisha na kuzisaidia familia hizi. Kujenga kuaminiana kutaanza na watu wa jamii husika.
- Wazazi wanataka watoto wao wakue wakiona na kufurahia utamaduni na lugha zao zinazothaminiwa na kutekelezwa katika mazingira ya elimu ya utotoni.

## Acknowledgements

AB Cultural Drivers — Responsive Evaluation & Research
ODI OSLC DEVELOPMENTS, Inc.
Portland State University
HAKI Community Organization — Humanitarian Assistance with Kindness & Interculturalism

*Funding for this work was provided by the Oregon Early Learning Division as part of the Preschool Development Grant. We would like to thank staff from the Humanitarian Assistance with Kindness & Interculturalism for agreeing to work with us to create an opportunity to hear from families. We are especially grateful to the families who took the time to share their experiences, needs, and hopes with us.*

*The project described was supported by Grant Number 90TP0020-01-02 from the Department of Health and Human Services Administration for Children and Families (DHHS). Its contents are solely the responsibility of the authors and do not necessarily represent the official views of DHHS.*